

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MJI WA URAMBO ("Urambo WSSA") KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21

Maombi ya mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-035

Mnamo tarehe 27 Agosti 2018, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Urambo (Urambo WSSA) la kutaka kuongeza bei ya huduma zake za majisafi kwa mwaka 2018/19 hadi 2020/21. Jedwali namba 1 hadi 5 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

Jedwali 1: Bei za Maji za sasa na zinazopendekezwa (shilingi kwa mita moja ya ujazo)

| Aina za Wateja | Matumizi (M3) | Bei za Sasa | Bei Zilizopendekezwa | | | | | |
|----------------|---------------|-------------|----------------------|---------|------------|---------|------------|---------|
| | | 2017/18 | % Badiliko | 2018/19 | % Badiliko | 2019/20 | % Badiliko | 2020/21 |
| Majumbani | | 800 | 30% | 1,040 | 6% | 1,102 | 9% | 1,201 |
| Taasisi | | 1,200 | 30% | 1,560 | 6% | 1,654 | 9% | 1,803 |
| Biashara | | 1,200 | 40% | 1,680 | 6% | 1,781 | 9% | 1,941 |
| Viwanda | | - | - | 2,500 | 6% | 2,650 | 9% | 2,890 |
| Kioski | Lita 20 | 30 | 33% | 40 | 25% | 50 | 20% | 60 |
| Bulk Customer | Lita 1,000 | 1,500 | 67% | 2,500 | 0% | 2,500 | 20% | 3,000 |

Jedwali 2: Gharama za Wateja Wasio na Dira za Sasa na Zilizopendekezwa (shilingi/mwezi)

| Aina za Wateja | Bei za Sasa | Bei Zilizopendekezwa | | | | | |
|----------------|-------------|----------------------|------------|---------|------------|---------|------------|
| | | 2017/18 | % Badiliko | 2018/19 | % Badiliko | 2019/20 | % Badiliko |
| Majumbani | 5,500 | 36% | 7,500 | 7% | 8,000 | 6% | 8,500 |
| Taasisi | 11,000 | 82% | 20,000 | 25% | 25,000 | 20% | 30,000 |
| Biashara | 11,000 | 127% | 25,000 | 20% | 30,000 | 17% | 35,000 |

Jedwali 3: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya (Shilingi kwa maunganisho mapya)

| Aina za Wateja | Bei za Sasa | | Bei Zilizopendekezwa | | | | |
|----------------|-------------|----------|----------------------|----------|---------|----------|---------|
| | 2017/18 | % | 2018/19 | % | 2019/20 | % | 2020/21 |
| | | Badiliko | | Badiliko | | Badiliko | |
| Majumbani | 15,000 | 0% | 15,000 | 33% | 20,000 | 0% | 20,000 |
| Taasisi | 15,000 | 0% | 15,000 | 33% | 20,000 | 0% | 20,000 |
| Biashara | 15,000 | 0% | 15,000 | 33% | 20,000 | 0% | 20,000 |
| Viwanda | 15,000 | 0% | 15,000 | 67% | 25,000 | 20% | 30,000 |

Jedwali 4: Bei za sasa na Zinazopendekezwa za Kuhamisha Maungio (Shilingi/Mwezi)

| Aina za Wateja | Bei za Sasa | | Bei Zilizopendekezwa kwa Miaka Mitatu | | | | |
|----------------|-------------|----------|---------------------------------------|----------|---------|----------|---------|
| | 2017/18 | % | 2018/19 | % | 2019/20 | % | 2020/21 |
| | | Badiliko | | Badiliko | | Badiliko | |
| Majumbani | 10,000 | - | 10,000 | 20% | 15,000 | 25% | 15,000 |
| Taasisi | 10,000 | - | 10,000 | 20% | 15,000 | 25% | 15,000 |
| Biashara | 10,000 | - | 10,000 | 20% | 15,000 | 25% | 15,000 |
| Viwanda | - | - | 10,000 | 20% | 15,000 | 25% | 15,000 |

Jedwali 5: Ada ya Huduma ya sasa na Zinazopendekezwa (Shilingi/mwezi)

| Aina ya Mteja | Bei za Sasa | | Ada Zilizopendekezwa kwa Miaka Mitatu | | | | |
|---------------|-------------|----------|---------------------------------------|----------|---------|----------|---------|
| | 2017/18 | % | 2018/2019 | % | 2019/20 | % | 2020/21 |
| | | Badiliko | | Badiliko | | Badiliko | |
| Majumbani | - | 0% | 500 | 50% | 750 | 33% | 998 |
| Taasisi | - | 0% | 500 | 50% | 750 | 33% | 998 |
| Biashara | - | 0% | 500 | 50% | 750 | 33% | 998 |
| Viwanda | - | 0% | 500 | 50% | 750 | 33% | 998 |

Kutokana na wasilisho la Urambo WSSA, bei zinazopendekezwa zitaiwezesha Mamlaka kuongeza mapato ili kumudu gharama za uendeshaji na matengenezo na pia kumudu gharama za ukarabati na kubadilisha miundombinu.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Jumatano, tarehe 05 Desemba, 2018, katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, Urambo Mjini** kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu ndani ya kipindi kabla ya **tarehe 19 Desemba, 2018**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana Makao Makuu ya EWURA, **GHOROFA YA NNE, JENGO LA LAPF, BARABARA YA MAKOLE**, au ofisi za Urambo WSSA zilizoko mjini Urambo.

**Imetolewa na:
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)
05 Novemba 2018**

